

KENYA Mass for July 15- SATURDAY

PRESIDER: FR. MAHOUSSI

1. Entrance:

Twimbe Kwa Shangwe Lyrics

Twimbe kwa shangwe na furaha *2
Bwana ametufanyia makuu

Tuingie kwake Mungu wetu,
Tuingie kwake kwa shukrani,
Bwana ametufanyia makuu

Yeye ndiye Mungu wa miungu,
Yeye ndiye Bwana wa mabwana,
Bwana ametufanyia makuu

Bwana ni mfalme wa wafalme,
Yeye ndiye Baba wa viumbi,
Bwana ametufanyia makuu

Ametenda mambo ya ajabu,
Aliye gizani hatajua,
Bwana ametufanyia makuu

Tuingie kwake Muumba wetu
Tuingie kwake kwa shukrani
Bwana ametufanyia makuu

Sifa na heshima kwake Mungu
Mwenye utukufu wa ajabu
Bwana ametufanyia makuu

2. UTUHURUMIE (MISA KARIOBANGI)

[v] Utuhurumie
[w] Ee Bwana, ee Bwana, ee Bwana

[v] Tuhurumie

[w] Ee Bwana, ee Bwana, ee Bwana, Bwana utuhurumie

Utuhurumie

Ee Kristu, ee Kristu, ee Kristu

Tuhurumie

Ee Kristu, ee Kristu, ee Kristu, Kristu utuhurumie

3. Bible Procession (Kenyan Style)

Inasonga Mbele Lyrics

Inasonga mbele injili yetu ulimwenguni kote -
Neno laenda mbele *2

Injili - (iende mbele Injili yake Yesu *2) *2
{ Inasonga mbele - Injili *2 yake Yesu *2 }

Inasonga mbele injili yetu katika mataifa -
Inasonga mbele injili yetu katika makabila -

Inasonga mbele Injili yetu katika jumuiya

Readings:

GOSPEL:

Homily: Margaret Gonsalves

4. Sadaka Beba Mikononi Lyrics

Tusimame ndugu twende kwake Bwana (kweli)
Usisite ndugu amka twende hima

Beba mikononi (mwako) ulijojaliwa
Peleka kwa Bwana, upate Baraka

Peleka kwa moyo, moyo wa mapendo (kweli)

Peleka kwa Bwana ulijojaliwa

Sadaka ya fedha, fedha za mifuko (ndugu)
Amka upeleke mezani kwa Bwana

Mavuno mifugo, ni mali ya Bwana (kweli)
Tupeleke kwake atazipokea

Mkate divai tupeleke kwake (leo)
Tupate baraka mbele zake Bwana

Twende ndugu twende, mbele zake Bwana (twende)
Tupeleke nafsi zetu kwake Bwana

5.Mtakatifu (miss Kariobangi)

[b] Mtakatifu

[w]: Mtakatifu Mtakatifu Bwana Mungu

[b] Wa majeshi

[w] Mbingu na dunia zimejaa tukufu wak
Hosanna, Hosanna juu Mbinguni

[Hosanna] Hosanna juu Mbinguni

Mbarikiwa

Anayekuja kwa jina lake Bwana Mungu

6. FUMBO LA IMANI (MISA KARIOBANGI)

Kristu - alikuwa, Kristu - alifufuka
Kristu Yesu - alikuwa, alifufuka, atakuja tena

7.BABA YETU (MISA KARIOBANGI)

Baba yetu uliye Mbinguni, Jina lako litukuzwe
Ufalme wako ufile utakalo lifanyike

Duniani kama Mbinguni -utakalo lifanyike
Tupe leo mkate wetu -
Mkate wetu wa kila siku -

Tusamehe makosa yetu -
Kama vile twawasamehe -
Waliotukosea sisi -
Situdie majaribuni -
Walakini utuopoe -
Maovuni utuopoe -
Kwa kuwa ufalme ni wako -
Na nguvu na utukufu -
Utukufu hata milele -

8.FE MWANA KONDOO (MISA KARIOBANGI)

[S] Ee Mwana kondoo

[w] Uondoaye dhambi za dunia utuhurumie } *2

Ee Mwanakondo . . .y

Ee Mwana kondoo

Uondoaye dhambi za dunia utujalie amani

9. COMMUNION

10.THANKSGIVING

Natamani Kuruka Lyrics

(Nipishe Njia)

Nipishe njia nipeni nafasi
Nimuonyeshe Mungu nilivyofurahi
Nitamwimbia ngoma nitacheza
Nimuonyeshe Mungu nilivyofurahi

Natamani kuruka, nifika kule
Nimuinue Mungu kwa mikono yangu
Nimueleze kwa kinywa, changu mwenyewe
Kwamba nimefurahi kwa upendo wake
Bwana nashukuru, nashukuru nashukuru tu
Ninashukuru kwa kunipenda bila mwisho

Sina cha kusema, cha kusema cha kusema tu
Ninashukuru kwa kunipenda bila mwisho

Kaniinua kutoka shimoni -
Akaniweka juu ya kinara -
Nitazunguka kwa maringo tele -
Na tabasamu lisilo kauka -

Nitawashika wenzangu mikono -
Tujjinue juu kwa pamoja -
Wenzangu si mmejionea wenyewe -
Mungu alivyo mwema wa ajabu -

Nitaandika utukufu wake -
Na wajukuu wangu wausome -

11.EXIT

Jina Maria Lyrics

Jina Maria jina tukufu lafurahisha latuliza
Hata malaika wanaliimba,
Ave ave Maria, Ave ave ave Maria
Wakisema (siku zote) bila mwisho
Ave Maria! Ave ave ave Maria

Jina Maria jina tukufu, lafurahisha la tutuliza
Jina Maria jina tukufu, latuletea neema ya Mungu
Jina Maria jina tukufu, lawafukuza pepo wabaya

Jina Maria jina tukufu, lawapendeza watakatifu